NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Riḍván 2019

Kwa Wabahá'i wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa sana,

Wakati Tamasha Kuu Kabisa likikaribia, tumehamalishwa kwa hisia za shukrani na matazamio—shukrani kwa maajabu ambayo Bahá'u'lláh amewawezesha wafuasi Wake kutimiza, matazamio ya kile siku za usoni hubeba.

Msukumo uliyofanyizwa na sherehe za kiulimwengu za miaka mia mbili ya Kuzaliwa kwa Bahá'u'lláh ndiyo kwanza tu umekua. Maendeleo yaliyochapuzwa ya jumuiya ya Kibahá'í, uinukaji wake wa uwezo, na werevu wake wa kuchota nguvu za wanajumuiya wake zaidi hujitokeza waziwazi kutokana na muhtasari wa mafanikio yake ya kiulimwengu ya hivi karibuni. Miongoni mwa haya, ongezeko la shughuli za ujenzi wa jumuiya hususani hujipambanua kipekee sana. Mpango wa Miaka Mitano wa sasa hufuatia miaka ishirini ya jitihada zilizofanywa na ulimwengu wa Kibahá'í kuboresha kiutaratibu na kuzidisha shughuli hizi—lakini ya kusifika, katika miaka miwili na nusu ya kwanza ya Mpango, idadi ya shughuli za msingi pekee iliinuka kwa zaidi ya nusu. Jumuiya ya kiulimwengu imeonesha uwezo kuwashirikisha, kwa wakati wowote ule, zaidi ya watu milioni moja katika shughuli hizo, ikiwasaidia kuchunguza na kuitika kwenye uhalisia wa kiroho. Katika kipindi hicho hicho kifupi, idadi ya mikusanyiko ya sala iliongezeka takribani mara mbili—muitikio uliohitajika zaidi kwa mifarakano ikuayo ya jamii ya binadamu kutoka Chanzo cha matumaini na majaliwa. Maendeleo haya hubeba ahadi maalum, kwani mikutano ya ibada hupenyeza ari mpya katika maisha ya jumuiya. Ikifumwa na jitihada za kielimu kwa rika zote, inaimarisha kusudi bora kabisa la jitihaza hizo: kukuza jumuiya zilizojipambanua kwa jinsi ya ibada yao kwa Mungu na huduma yao kwa wanadamu. Hii haidhihiriki zaidi popote kuliko katika zile klasta ambako ushiriki wa idadi kubwa katika shughuli za Kibahá'í unadumishwa na marafiki wamepita hatua ya tatu ya ukuaji katika maendeleo yao ya kijamii. Tumefurahishwa kuona kwamba idadi ya klasta ambako mchakato wa ukuaji umepiga hatua kwa kiwango hiki tayari zimezidishwa zaidi ya mara mbili tangu kuanza kwa Mpango na sasa zipo kwenye mia tano hivi.

Mapitio haya mafupi hayawezi kutendea haki kiwango cha mabadiliko ambayo yanaendelea. Matazamio kwa miaka miwili iliyobakia ya Mpango ni yenye kutia moyo. Mengi yametimizwa kwa mwaka huu uliopita kwa kueneza kwa mapana ujifunzaji kutoka katika program imara za ukuaji katika klasta ambazo, kama tulivyotarajia, zimekuwa bwawa la maarifa na rasilimali. Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, Washauri, na wasaidizi wao wasiochoka hawakuzuiwa na chochote kuhakikisha kwamba marafiki katika sehemu zote za ulimwengu wanaweza kunufaika kutokana na uchapuzaji huu katika kujifunza na kutumia umaizi unaopatikana kwenye uhalisia

wao wenyewe. Tunafurahi kuona kwamba katika idadi iongezekayo ya klasta, na katika ujirani na vijiji vilivyomo ndani mwake, kiini cha marafiki kimeibuka ambao kwa kupitia utendaji na tafakari wanagundua kile kinachohitajika, kwa wakati maalum, ili mchakato wa ukuaji usonge mbele katika mazingira yao. Wanachota kwenye chombo chenye nguvu, taasisi, ambapo kupitia kwacho uwezo wa kuchangia kwenye ustawi wa kiroho na kimwili wa jumuiya huchochewa, na wakati watendapo, idadi ya wale wanaojumuika nao inaongezeka. Kwa kawaida, hali hutofautiana kwa kiasi kikubwa kutoka sehemu moja hadi nyingine, kama ilivyo kwa sifa bainifu za ukuaji. Lakini kwa kupitia upambanaji wa kiutaratibu, kila mmoja anaweza kutoa mchango unaofaa zaidi na zaidi kwa kazi iliyopo mbele yetu. Katika kila hali, kuna shangwe takatifu katika kuzishirikisha roho zingine katika mazungumzo yenye maana na yainuayo moyo ambayo husababisha, ama kwa haraka au taratibu, msisimko wa athari za kiroho. Kadiri mwali uliowashwa katika moyo wa muumini ulivyo mwangavu zaidi, ndivyo itakavyokuwa kubwa zaidi nguvu ya mvuto ihisiwayo na wale wanaopata joto lake. Na kwa moyo ulioteketezwa kwa upendo wa Bahá'u'lláh, ni kazi gani ifaayo zaidi inayoweza kufikiriwa kuliko kutafuta moyo wa undugu, kuwatia moyo kadiri waingiavyo katika njia ya huduma, kuambatana nao kadiri wapatavyo tajiriba na—pengine shangwe kuu kabisa ya zote—kuona roho zikithibitishwa katika imani yao, zikiinuka kwa kujitegemea, na kuwasaidia wengine kwenye safari hiyo hiyo. Haya ni miongoni mwa mambo yahusudiwayo kabisa kushinda yote ya nyakati zote ambapo maisha haya ya mpito hudiriki.

Matarajio kwa ajili ya kuendeleza shughuli hii ya kiroho yanafanywa ya kusisimua zaidi kwa kukaribia kwa sherehe ya miaka miambili ya Kuzaliwa kwa Báb. Kama ilivyokuwa sherehe ya miaka mia mbili iliyoitangulia, maadhimisho haya ni wasaa wa thamani isiyopimika. Yanawapa Wabahá'í wote fursa za ajabu kwa ajili ya kuwaamsha wale walio karibu yao kwenye Siku ya Mungu, kwenye mmiminiko usio wa kawaida wa rehema za mbinguni zilizoashiriwa kwa utokeaji wa Wadhihirishaji wawili wa Kiumbe Mtakatifu, Nyota chanjari Ambao waliuangazia upeo wa ulimwengu. Kiwango cha kile kinachowezekana katika duru mbili zijazo kinajulikana kwa wote kutokana na tajiriba ya sherehe za miaka mia mbili miaka miwili iliyopita, na yale mafunzo yote yaliyopatikana katika tukio lile lazima yaelekezwe katika mipango kwa ajili ya Sherehe Pacha za Kuzaliwa za mwaka huu. Kadiri maadhimisho ya miaka mia mbili yanavyokaribia, tutafanya maombi ya mara kwa mara kwa niaba yenu katika Makaburi Matakatifu, tukisali kwamba jitihada zenu za kumuenzi Báb istahilivyo zitafanikiwa katika kuendeleza Hoja Aliyoibashiri.

Mwisho wa karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi ni miaka miwili na nusu tu kutoka sasa. Itahitimisha miaka mia moja ya jitihada za wakfu kuimarisha na kupanua msingi uliowekwa kwa kujitoa dhabihu kabisa wakati wa Zama za Kishujaa za Imani. Wakati huo jumuiya ya Kibahá'í pia itaadhimisha miaka mia moja ya Kupaa kwa 'Abdu'l-Bahá, ndiyo wakati ule ule ambapo Bwana aliachiwa huru kutokana na mipaka ya ulimwengu huu kwenda kuungana na Baba Yake katika viunga vya utukufu wa mbinguni. Maziko Yake, ambayo yalifanyika siku iliyofuata, lilikuwa ni tukio "ambalo mfano wake Palestina ilikuwa haijahi kushuhudia kamwe". Kwenye hitimisho lake, mabaki Yake ya umauti yalipumzishwa ndani ya kuba ya Kaburi kubwa, zuri la Báb. Walakini, ilitaamaliwa na Shoghi Effendi kwamba huu ungekuwa ni utaratibu wa muda tu. Kaburi Takatifu lilikuwa liinuliwe, lenye sifa zinazolistahili daraja la kipekee la 'Abdu'l-Bahá, kwa wakati muafaka.

Wakati huo umewadia. Ulimwengu wa Kibahá'í unaitwa kujenga jumba ambalo milele litayakumbatia yale mabaki matakatifu. Litajengwa katika viunga vya Bustani ya Riḍván, kwenye ardhi iliyowekwa wakfu na nyayo za Uzuri Uliobarikiwa; Kaburi Takatifu la 'Abdu'l-Bahá hivyo litakuwa kwenye hilali iliyopo kati ya Makaburi Matakatifu huko 'Akká na Haifa. Kazi ya mipango ya usanifu inaendelea, na taarifa zaidi itatolewa katika miezi ijayo.

Hisia za furaha ya kupita kiasi hivi sasa zinafura ndani mwetu, kadiri tunavyotafakari mwaka ulio mbele yetu na yale yote unayoyatarajia. Tunatazamia kwa kila mmoja wenu—wale wajishughulishao na utoaji wa huduma kwa Bahá'u'lláh, wakifanya kazi katika kila taifa kwa ajili ya hoja ya amani—kutimiza wito wenu mkuu.

*NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU*